BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA

## MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**,

Nomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma na utukufu, kwa kutujaalia uzima na Afya njema iliyotuwezesha kukutana kwa mara nyengine tena asubuhi ya leo ndani ya Baraza hili Tukufu, kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Seriakali na Taasisi zake. Aidha, kwa dhati kabisa nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa kuhusu ***Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025.*** Ninamuomba Mwenyezi Mungu akupe nguvu na Imani thabit ya kuliongoza Baraza hili kwa hekma na uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa umuhimu wake, natoa shukrani na pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa namna anavyosimamia vyema ahadi zake anazozitoa katika uongozi wake kwa kuyaweka maslahi ya watumishi wa umma yazidi kuimarika.

Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hii ni matokeo mazuri ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambayo utekelezaji wake utaendelea kwa kipindi chote cha Bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa kuona hatua kubwa ya maendeleo inafikiwa itakayoiwezesha jamii kiuchumi na kujikwamua na umasikini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kipekee, napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati Makamu wa Kwanza Rais Mheshiwa Masoud Othaman Masoud kwa namna bora anayomsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake. Aidha, nimpongeze Waziri katika Ofisi hii ambaye ni Mheshimiwa Harusi Said Suleimain, akisaidiwa na Katibu Mkuu wake Dkt. Omar Dadi Shajak pamoja na Afisa Mdhamini Pemba, na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa kwenye utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/2024 na kwa msaada wao mkubwa walioionesha Kamati katika kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**,

Nitakuwa sijatenda haki iwapo sijaipongeza Kamati hii kwa kazi kubwa walioifanya wajumbe wenzangu wakati tukiwa tunapitia bajeti ya fungu hili na kuonesha mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi zaidi. Hivyo, kwa ridhaa yako naomba niwatambue wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Thani Juma | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Panya Ali Abdallah | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 10. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 11. | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| 12. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika**,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeweza kuchambua na kujiridhisha vyema wakati ikipitia Mafungu ya Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 97(1) na 107(3) kwenye jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2020. Kwa ruhusa yako, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati kwa Programu zote ambazo Kamati yangu imezitolea ushauri na maelekezo kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika**,

Katika kutekeleza kazi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imefanikiwa kutembelea na kujionea shughuli mbali mbali za kawaida na zile za miradi ya maendeleo ambazo zinasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia program zake. Kiujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa shughuli za Bajeti kwa Ofisi hii ambayo imeundwa na baadhi ya Taasisi zinazojitegemea kupitia Mafungu manne ya kibajeti ambayo ni:- B01 Fungu la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Ofisi Kuu; B04 - Fungu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA); C04 Fungu la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na C05 Fungu la Tume ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Fungu la B01 lina Programu Kuu nne ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi; Programu ya Watu wenye Ulemavu; Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa ***Program Kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi*** ambayo inasimamia sera, sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ya Kimataifa kuhusiana na mazingira hapa nchini na Ulimwenguni kwa ujumla, kimsingi Kamati hii hairidhishwi na ushiriki mdogo wa Zanzibar katika mikutano na makongamano ya kimataifa ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ambayo yanafanyika kila mwaka katika nchi mbalimbali Duniani. Kwa mfano mwaka 2023 katika mkutano wa Cop 28 uliofanyika Dubai, Zanzibar ilipeleka washiriki wachache mno ukilinganisha na Tanzania bara ambayo ilipeleka washiriki zaidi ya 600 katika fani mbali mbali. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuweka nguvu ya ushiriki wa Wazanzibari katika mikutano hiyo kwa kuwa na ushiriki mkubwa ili waweze kuisaidia jamii kupata elimu ya mazingira na kufahamu mipango ya Ulimwengu kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia, inaipongeza Idara ya Mazingira kwa kuweza kufanya tathmini ya mazingira na kutoa ripoti inayoonesha maeneo mbali mbali yaliyoathirika kutokana na shughuli za kimaumbile na zile za kibinadamu, na kushauri kuwa maeneo haya yanahitaji kuchukuliwa hatua za haraka na za kimkakati ili kuinusuru nchi yetu na majanga makubwa zaidi ya ukame na njaa. Kwa mnasaba huo, ili programu hii iweze kutekelezwa Serikali inapaswa kusimamia kikamilifu upatikanaji wa fedha ambazo zitakuwa mkombozi katika kufikia hatua ya mafanikio.

**Mheshimiwa Spika**,

Vile vile, kamati inaipongeza Ofisi kwa kuendelea kuimarisha masuala ya watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutoa uelewa juu ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Nam. 8/2022 na kuifanya jamii iweze kutambua na kuthamini mchango wa watu wenye ulemavu katika mazingira yetu. Hata hivyo, Kamati inaiomba Serikali kurekebisha Kanuni zake za mikopo kupitia Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ili kuwafanya Watu wenye Ulemavu kupatiwa mikopo kwa unafuu badala kulazimika kupatiwa mikopo hiyo kwa njia vikundi kwani kutokana na idadi wa jamii ya watu hawa waliopo Zanzibar ni vigumu kuweza kupata vikundi vya watu wenye ulemavu kwa kila mtaa au kitangoji. Serikali ikizingatia suala hili kwa muonekano mpana kutasaidia kunyanyua hali za watu wenye ulemavu kiuchumi na kuweza kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, kamati inalipongeza Baraza la Watu Wenye Ulemavu kwa kupata Muundo mpya wa kitaasisi ili sheria yao iweze kupata nguvu na kusimamiwa kikamilifu. Kamati inaliomba Baraza kuharakisha utekelezaji wa muundo huo kwa kuwaweka watendaji kwa madaraja yanayostahili. Sambamba na hilo, Kamati inazitaka Wizara na taasisi za umma kuhakikisha wanawajali Watu wenye Ulemavu katika utekelezaji wa majukumu yao ya msingi kwa kuzingatia miundombinu iliyobora ndani ya ofisi zao pamoja na kutoa kipaumbele cha ajira, pamoja na kutiliwa mkazo utoaji wa elimu mjumuisho. Aidha, Kamati inatia msisitizo kwa Baraza kusimamia na kuzifanyia kazi ofisi za Wilaya ili kusaidia kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu kiurahisi na kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Moja ya malengo waliyojiwekewa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa **Fungu B04** yenye **Programu ya Usimamizi wa Mazingira** ni kuendeleza kusimamia

utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya kimazingira; Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikisha Ujenzi wa matuta yenye ukubwa wa 119m3 kwa ajili ya kuzuia mmong'onyoko wa udongo pamoja na kufanikiwa kutoa miongozo ya kimazingira ambayo imesaidia kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira wa maeneo mbali mbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inaishauri Serikali kuandaa mradi utakaosaidia kuzuia mmong'onyoko wa ardhi pembezoni mwa bahari kuanzia maeneo ya Ocean View Mnara wa Mbao mpaka katika eneo la nyumba ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Mazizini kwani maeneo haya yapo hatarini kupoteza uwasili wake kutokana na mmong'onyoko mkubwa ambao husababishwa na maji ya mvua yanayotiririka kutoka juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati wakati ikifanya ziara zake za kawaida imegundua maeneo mbali mbali yameathiriwa kutokana na uharibifu wa mazingira unaoendelea siku hadi siku ikiwemo uchimbaji wa mchanga na ukataji wa matofali ya mawe bila mpangilio katika maeneo ya Micheweni na uchimbaji wa mawe kiholela unaofanywa maeneo mbali mbali hususan katika ukanda wa bahari. Kwa hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia bajeti ya mwaka huu kutafuta njia bora ya kuwasaidia na kuwajali wananchi wanaojishughulisha na biashara hizi za uharibifu wa mazingira ili waweze kujiajiri katika shughuli nyengine na kuhakikisha sehemu zilizoathiriwa zinapandwa miti kwa ajili ya kuirudisha ardhi katika hali yake ya asili.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, kamati inaitaka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iwapo fedha walizoziomba **Shilingi Bilioni 1.83/-** wataidhinishiwa kuweka mkazo suala la utoaji wa elimu zaidi kwa jamii ili kuzuia uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaoendelea katika shehia zetu, pamoja na kuwachukuliwa hatua za kisheria wale wote ambao kwa makusudi wanapingana na utekelezaji wa miongozo ya kimazingira inayotolewa na taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa udhibiti na uendelezaji wa mapambano juu ya usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya linalosimamiwa na **Fungu C04.** Kamati imeridhishwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha suala hili linadhibitiwa ipasavyo ikiwa pamoja na kukamilisha marekebisho ya Sheria Nam. 8/2021 ya Kudhibiti na Kupambana na athari Dawa za kulevya kwa baadhi ya vifungu pamoja na kanuni zake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia hotuba ya bajet ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka 2024/2025, kamati inaipongeza Mamlaka kwa kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa mwenye kiwango kikubwa cha dawa za kulevya chenye uzito wa 105kg (Hashishi 67kg, Skanka 34kg, Methamphetamine 2kg na Heroin 2kg). pia, Kamati inaishukuru na kuipongeza sana Mamlaka kwa kuzidisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya kutokana na kutaifisha mali za mhusika mkuu wa Dawa za Kulevya ambaye kwa kiasi kikubwa amekuwa akihusika na uingizaji na usambazaji wa dawa kutoka nje na kuathiri kundi kubwa la vijana wetu hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa moyo wa dhati kabisa, kamati inatoa pongezi kwa  Mamlaka kufuatia Ujenzi wa jengo la uendeshaji wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni kwani kumalizika kwa kituo hicho kutatoa fursa kwa waraibu wengi kurekebishwa tabia na kuirudisha nguvu ya taifa ya vijana ambao kwa kasi wanaangamia kutokana na utumiaji wa dawa za kulevya. Mbali na pongezi hizo, Kamati inaitaka Mamlaka kupitia fedha watakazoidhinishiwa kwa mwaka huu 2024/2025 kutafuta mbinu madhubuti za kutokomeza janga hili lisiweze kuendelea, kujipanga kwa ajili ya ununuzi wa samani za kituo hicho pamoja kuanza ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa upande wa Pemba baada ya ujenzi wa Kituo cha Unguja kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,**

Jukumu la msingi la kuratibu na kusimamia muitiko wa taifa dhidi ya UKIMWI ni kuweka miongozo ya kitaifa na mikakati ya kudhibiti maambukizo mapya ya VVU katika jamii. Kupitia Programu kuu za **Fungu C05** kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia ofisi ya Tume ya Ukimwi kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa inazingatia makundi ya vijana, wanawake na makundi maalum ambayo yana ambukizwa zaidi. Kamati kupitia bajeti hii inaishauri Serikali kuwatafutia jengo la Kudumu la Tume ya Ukimwi ili kupunguza fedha za kodi ambazo hulipwa kila mwezi kwa ajili ya matumizi ya ofisi yao ya sasa hapo Mombasa kwa Mchina.

**Mheshimiwa Spika:**

Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni. Kamati inatoa shukrani za dhati kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Maselem, pamoja na watendaji wote kwa

ujumla wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ambao wamesaidia sana Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika:**

Mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie Bajeti hii na hatimae waidhinishe Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais makadirio ya mapato na matumizi ya fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati yangu

**Naomba Kuunga Mkono Hoja.**

Ahsante,

……………………………

(Machano Othman Said)

**MWENYEKITI,**

**Kamati za Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**